

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
(VETA)**

**MKATABA WA KUUZA, KUTENGENEZA NA KUFUNGA ALLUMINIUM MADIRISHA YA
CHUO CHA WILAYA YA UKEREWE**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 07 mwezi Februari, 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA Mwanza, S.L.P 1983, Mwanza, ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

TAWAQAL SEIF SAMBILO S.L.P. 11001 MWANZA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Muuzaji Mtengenezaji na Mfungaji wa madirisha ya Alluminium") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri anasimamia Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Wilaya Ukerewe (Ukerewe DVTC);

KWA KUWA Mwajiri amekubaliana na Muuzaji wa vifaa, mtengenezaji na mfungaji wa vifaa vya alluminium kuuza, kutengeneza na kufunga madirisha ya alluminium katika chuo cha Veta cha Wilaya ya Ukerewe.

KWA KUWA Mwajiri amempatia Muuzaji wa vifaa, Mtengenezaji na Mfungaji wa madirisha ya Alluminium orodha ya madirisha ya Alluminium yanayotakiwa kutengenezwa na kufungwa katika chuo cha Veta cha Ukerewe.

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Gharama ya kuuza, kutengeneza na kufunga itakuwa ni Tshs 144,610,000.00 , kiasi hiki cha Fedha kitajulikana kama "Gharama ya kuuza kutengeneza na kufunga " kama mchanganuo wa unavyoonesha:

No.	Item Description	Qty	Unit	Rate	Amount
1	Aluminum sliding window 100mm wide 2mm thick bronze, anodized aluminum window complete with grazing sliding mosquito gauze and all necessary iron mongeries 2000x1850mm High	18	pcs	700,000.00	12,600,000.00
2(a)	1500x1850mm High	4	pcs	660,000.00	2,640,000.00
(b)	2000x1350mm High	1	pc	660,000.00	660,000.00
3	1200x1350mm High	2	pcs	360,000.00	720,000.00
4	800x1350mm High	8	pcs	280,000.00	2,240,000.00
5	3770x2200mm High	11	pcs	1,500,000.00	16,500,000.00
6	2870x1820mm High	42	pcs	790,000.00	33,180,000.00
7	3770x1820mm High	6	pcs	1,200,000.00	7,200,000.00
8	1000x600mm High	18	pcs	230,000.00	4,140,000.00
9	2000x600mm High	6	pcs	290,000.00	1,740,000.00
10	1600x1800mm High	1	pcs	680,000.00	680,000.00
11	800x950mm High	2	pcs	260,000.00	520,000.00
12	4770x950mm High	4	pcs	760,000.00	3,040,000.00
13	1500x1600mm High	36	pcs	480,000.00	17,280,000.00
14	2700x900mm High	4	pcs	500,000.00	2,000,000.00
15	2400x900mm High	2	pcs	440,000.00	880,000.00
16	900x900mm High	8	pcs	310,000.00	2,480,000.00
17	2670x2100mm High	3	pcs	800,000.00	2,400,000.00
18	2500x2100mm High	17	pcs	790,000.00	13,430,000.00
19	2500x1200mm High	2	pcs	680,000.00	1,360,000.00
20	1200x1200mm High	4	pcs	320,000.00	1,280,000.00
21	2400x900mm High	1	pc	440,000.00	440,000.00
22	1500x2100mm High	2	pcs	750,000.00	1,500,000.00
23	1800x2100mm High	3	pcs	700,000.00	2,100,000.00
24	1500x1800mm High	11	pcs	660,000.00	7,260,000.00
25	1200x1800mm High	4	pcs	440,000.00	1,760,000.00
26	900x1800mm High	2	pcs	360,000.00	720,000.00
27	800x600mm High	2	pcs	180,000.00	360,000.00
28	Curtain wall 6700x2400mm	1	Pc	3,500,000.00	3,500,000.00
Total					144,610,000.00

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA USAFIRISHAJII (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)
Gharama ya kuuza, kutengeneza, na kufunga madirisha ya Alluminium haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya usafirishaji yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa mmuzaji, Mtengenezaji na mfungaji wa madirisha ya Alluminium kwa mfumo wa mkataba ndani ya siku saba baada ya kuanza kazi na malipo yatalipwa kwa awamu mbili.

- (a) Malipo ya awamu ya kwanza 50% ya gharama yote
- (b) Malipo ya awamu ya pili 45% ya gharama yote
- (c) Retention money 5%

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Muuzaji, mtengenezaji na mfungaji ataanza kutengeneza madirisha ya Alluminium kuanzia tarehe 14.02.2022

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Muuzaji, mtengenezaji na mfungaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA MUUZAJI, MTENGENEZAJI NA MFUNGAJI

Muuzaji, mtengenezaji na mfungaji atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kuuza, Kutengeneza na kufunga madirisha ya alluminium na kukabidhi kwa Afisa ugavi na Msimamizi wa mradi wa chuo cha Wilaya ya Ukerewe.
- (b) Kuhakikisha kazi ya kutengeneza na kufunga Madirisha ya Alluminium inafanyika kwa ubora zaidi na kwa kiwango bora.

WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kumlipa Muuzaji, mtengenezaji na mfungaji malipo halali ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu
- (b) Kumkata kodi ya zuio (withholding tax).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA MWANZA.

Jina: MAPAMBA L.A.M Saini: _____

Wadhifa: Aj. Principal Tarehe: 07/02/2022



Mbele ya (Shahidi)


Jina: Roderick James Mita Saini: _____

Wadhifa: Director - Mbari Tarehe: 07/02/2022

IMESAINIWA NA MUUZAJI, MTENGENEZAJI NA MFUNGAJI

Jina: TAWAQAL SEIF SAMBIRO Mbele ya _____ Saini: _____

Wadhifa: DIRECTOR Tarehe: 07/02/2022



Mbele ya (Shahidi)

Jina: Ayoub Shaban Hassan Saini: _____

Wadhifa: G. MANAGER Tarehe: 07/02/2022